

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Telegrams "AFYA", DODOMA
Nambari ya simu: 255-026-2323267/2351196
Fax Na.255-22-213806



Mji wa Serikali - Mtumba,
Barabara ya Afya,
S. L. P 743,
40478 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

**TAARIFA YA TETESI ZA UWEPO WA MGONJWA MWENYE DALILI ZA
UGONJWA WA HOMA YA MAFUA MAKALI UNAOSABABISHWA NA KIRUSI
KIPYA AINA YA CORONA (Novel Corona Virus 2019-nCoV) KATIKA KIWANDA
CHA SUNDA TAWI LA ARUSHA NA TAHADHARI YA UGONJWA HUO HAPA
NCHINI.**

Arusha, Jumatatu Januari 28, 2020.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, inapenda kutoa taarifa na tahadhari kwa umma kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mafua makali uliozikumba nchi za China, Thailand, Japan, Korea ya Kusini na Marekani kuanzia mwazoni mwa mwezi Desemba 2019, ambapo Wizara imekuwa ikifuatilia kwa karibu mwenendo wa mlipuko wa ugonjwa huo tangu ulipotokea.

Pamoja na elimu na taarifa zinazotolewa na Wizara kila wakati kupitia njia mbalimbali vikiwemo vyombo vya habari, matamko rasmi na taarifa hizi kwa Umma bado kuna taarifa ambayo sio ya kweli inayosambaa kwenye mitandao ya jamii kuhusu tetesi ya kuwepo mgonjwa anaesadikiwa kuwa na ugonjwa huo unaosababishwa na kirusi tajwa hapo juu aina ya Corona.

Wizara baada ya kupata taarifa hii, kupitia Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha (Dkt.Sichwale), iliunda timu ya wataalam wakiwemo kutoka Jiji la Arusha, kumfuatilia msadikiwa huyu kwa haraka. Aidha, ilibainika mhisiwa huyu kuwa ni mchina (mwekezaji) ambaye alipatwa na mafua na chafya, lakini hakuwa na homa wala kikohozi.

Uchunguzi uliendelea na kadri muda ulivyosonga hali yake iliendelea kuimarika na hadi sasa anaendelea vyema na shughuli zake huku wataalamu wakiendelea kumfuatilia kama kutakuwa na mabadiliko yoyote.

Tunazidi kuwasihi watoa huduma wote katika maeneo ya kutolea huduma za jamii/ jumuiya kama mahoteli, migahawa, maduka ya huduma mbalimbali, sehemu za mikusanyiko mikubwa ya watu, watoa huduma na wenye vyombo vya usafiri wa jumuiya na wenye kufanana na makundi haya, kuendelea kuzingatia elimu inayotolewa na kutoa taarifa ya mhisiwa yeyote atakayeonekana kuwa na dalili tajwa hapa chini:-

Homa na mafua makali, kuumwa na kichwa, mwili kuchoka, kikohozi, kubanwa mbavu, maumivu ya misuli, vidonda vya koo, kuathiri mapafu, kupumua kwa shida na hata kifo.

Ugonjwa huu hauna chanjo wala tiba ya moja kwa moja, hivyo kama yalivyo magonjwa mengi yanayosababishwa na virusi, matibabu hufanyika kwa kuzingatia dalili zilizopo kwa ufuatiliaji mkubwa.

Ugonjwa huu huambukizwa kwa njia ya hewa kwa kuingiwa na majimaji yenye virusi kutoka mtu mmoja kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya au kwa kugusa majimaji au makamasi kutoka kwa mgonjwa aliyethibitishwa kuwa na ugonjwa huo.

MPAKA SASA TANZANIA HAINA MGONJWA. Wizara inapenda kutoa tahadhari kwa wananchi wote hususani ambao wanasafiri kwenda kwenye Mataifa yaliyoathirika na mlipuko wa ugonjwa huo na wale wanaopokea wageni kutoka katika nchi hizo.

Hivyo Wananchi wote wanashauriwa kuchukua hatua zifuatazo ili kujikinga na ugonjwa huu:-

- Kuzingatia kanuni za afya na usafi ikiwa ni pamoja na kukaa mbali na mtu mwenye dalili za mafua mwenye historia ya kusafiri katika nchi zilizokumbwa na mlipuko au mwenye dalili zilizotajwa hapo juu;
- Kufunika mdomo na pua wakati wa kukohoa kwa kitambaa safi au nguo uliyovaa sehemu za mikono;

- Kuepuka kugusana na mgonjwa mwenye dalili za magonjwa ya njia ya hewa;
- Kuzingatia usafi binafsi ikiwemo kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni;
- Kuwahi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya endapo utakuwa na dalili zilizoainishwa;
- Kutoa taarifa kwenye kituo cha huduma za afya kilicho karibu uonapo mtu mwenye dalili za magonjwa ugonjwa huo.

Wananchi wanashauriwa kutokuwa na hofu na hivyo waendeleo kuchukua tahadhari.

Imetolewa na:



Gerard J. Chami,

Mkuu Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali,

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - Afya